UCLA Library

Mpango wa Ulimwengu wa Uhifadhi wa Kisasa wa Urithi wa Utamaduni

Modern Endangered Archives Program (MEAP) ni mpango wa utoaji ruzuku wa Maktaba ya UCLA. Tunafadhili miradi ambayo inaweka kumbukumbu vizuri, inayohifadhi vitu vya zamani vya tangu karne ya 20 na 21 katika mfumo wa kidijitali, na kuhakikisha vitu hivyo vinapitakana. Vitu hivi viko katika hatari ya kuangamia na vinajumuisha vitu vilivyochapishwa, picha, filamu, sauti zilizonaswa, vitu visivyodumu, na vya kidijitali.

Maombi ya kikundi cha 4 yatafunguliwa Septemba 2021.

UFADHILI KATIKA KIWANGO CHA DUNIA NZIMA

Tunawahimiza watu kutoka Afrika, Visiwa vya Karibi, Amerika ya Kilatini, Mashariki ya Kati, Asia ya Kati, Asia ya Kusini na ya Kusini-Mashariki na Oceania watume maombi.

Mwongozo wa mpango na maelezo ya maombi yanapatikana katika lugha mbalimbali.

TUMIA MITINDO YENYE MAADILI

MEAP inaunga mkono kazi katika maeneo ya makavazi ulimwenguni kote, ikiwezesha wahifadhi-nyaraka na viongozi wa jamii kufafanua vipaumbele vya kazi zao za uhifadhi.

Mitindo ya baada ya utunzaji inaunda nyaraka zilizo na uwiano bila kusafirisha vitu.

HAKIKISHA ZINAWEZA KUFIKIWA KWA URAHISI

MEAP imejitolea katika uhifadhi wa kudumu + ufikivu endelevu wa nyaraka zilizofadhiliwa.

Vifaa vinaweka kumbukumbu ya historia, jamii, utamaduni, na siasa, na kutilia mkazo haki ya jamii, haki za kibinadamu, na jamii ambazo hazijasajiliwa.

UCLA Library

Modern Endangered Archives Program (MEAP)

Mradi wa Maktaba ya UCLA

Ufadhili unapatikana kwa kuweka kumbukumbu na uhifadhi wa urithi wa utamaduni ulio katika hatari kupitia kuwekwa katika mfumo wa kidijitali.

Maelezo yote yanapatikana kwenye meap.library.ucla.edu.

MWITO WA MAOMBI (2021-2022)

MEAP inakaribisha maombi ya miradi iliyoundwa kuhifadhi, kuweka kumbukumbu, na kuweka katika mfumo wa kidijitali nyaraka zote zilizo katika hatari inayotokana na hali ya mazingira, wasiwasi wa kisiasa, vyombo vya habari visivyo endelevu, uhifadhi usiofaa, au mabadiliko ya jumla au kijamii. Vifaa vyote vya kidijitali vilivyotengenezwa kupitia miradi ya MEAP vitachapishwa mtandaoni na Maktaba ya UCLA.

Maombi yataanza Septemba 10, 2021
Maombi ya awali yatatarajiwa Novemba 15, 2021

Maombi yote lazima yawasilishwe kupitia mfumo wa maombi wa mtandaoni wa MEAP unaopatikana meap.smapply.io. Iwapo huwezi kuufikia mfumo wa mtandaoni au huwezi kuwasilisha mtandaoni, tafadhali tuma barua pepe kwa meap@library.ucla.edu. Jifunze mengi zaidi katika meap.library.ucla.edu

RUZUKU INAYOPATIKANA

MEAP inatoa aina mbili za ruzuku. Aina zote mbili za ruzuku zinahitaji uwasilishaji wa maombi ya awali kupitia mfumo wa maombi wa MEAP. Waombaji watakaochaguliwa watakaribishwa kukamilisha maombi yenye maelezo zaidi.

Miradi lazima iwe na mpangilio mzuri kabla ya kuwekwa katika mfumo wa kidijitali. Iwapo unahitaji muda zaidi kutathmini na kukagua vifaa vya makavazi, sharti ufikirie kuhusu kutuma ombi la kupewa ruzuku ya upangaji.

RUZUKU YA UPANGAJI ya hadi $15,000 ya kutathmini au kukagua nyaraza ili ziwekwe katika mfumo wa kidijitali na/au upangaji. Miradi inayopokea ruzuku ya upangaji inawezakuwa hadi mwaka mmoja.

RUZUKU YA UPANGAJI inayofika $50,000 ya kubadilisha makavazi katika mfumo wa kidijitali au kupanga vifaa vilivyo katika mfumo wa kidijitali. Miradi iliyofadhiliwa na ruzuku inafaa kushughulikia kikamilifu harakati za kubadilisha katika mfumo wa kidijitali, ikiwemo

utaswirishaji pamoja na maelezo ya yaliyomo na upelekaji wa vifaa vya kidijitali kwa Maktaba ya UCLA. Ruzuku ya miradi inaweza kuwa hadi miaka miwili.

MEAP ina pesa zilizotengwa kwa Ruzuku ya Dharura itakayopewa nje ya mzunguko wa kawaida wa ufadhili. Pesa zinazofika $10,000 zinapatikana kwa miradi ya miezi 6. Maswali yanapaswa kutumwa kwa meap@library.ucla.edu. Maombi ni lazima yawe yamealikwa na yatafuata mchakato mkali wa kuyatathmini, ikiwemo uchunguzi wa mwamuzi wa nje, wataalamu wa kifundi, na bodi ya uchunguzi ya MEAP.

KUSTAHILI

Miradi ni lazima iwe na mwombaji mmoja mkuu anayechukua jukumu la upangaji na utekelezaji wa mradi. Mwombaji mkuu pia atakuwa na jukumu la udhibiti wa fedha za ruzuku. Waombaji wa kibinafsi lazima wawe na ushirikiano na taasisi na hawawezi kutuma ombi bila kuwa na uhusiano wowote. Iwapo mwombaji wa ruzuku hana uhusiano na umiliki wa uwekaji wa vifaa, ni lazima kuwe na barua ya kuunga mkono kutoka kwa umiliki wa uwekaji.

WAOMBAJI WANAOSTAHILI:

- Mshiriki yeyote aliyeidhinishwa wa kitivo cha kufunza au kutafiti katika chuo kikuu au taasisi nyingine inayofanana ya elimu ya juu
- Wahifadhi-nyaraka na wasimamizi wa maktaba walio na majukumu katika kitengo cha nyaraka maalum katika makavazi, maktaba ya kitaifa au ya utafiti, au taasisi kama hiyo
- Viongozi wa usimamizi katika mashirika yasiyo ya faida ambayo yana vifaa vya urithi wa utamaduni vilivyo katika hatari

TAASISI ZINAZOSTAHILI:

- Ruzuku lazima isimamiwe na mashirika yasiyo ya faida
- Maombi kutoka kwa taasisi za kitaifa zinazoomba ufadhili wa uhifadhi wa vifaa vyao yanafaa kuonyesha mchango usio wa pesa, kama vile utoaji wa mpango wa muda wa wafanya kazi, mafunzo au mahali pa kufanyia kazi.
- Taasisi ambazo ni mwenyeji sharti ziwe ni chuo kikuu, makavazi, maktaba, taasisi ya utafiti au ya utamaduni

UPEO WA MRADI

MEAP itasaidia miradi kuweza kupanga, kukusanya, kubadilisha, na kuelezea nyaraka au vifaa vya kidijitali vilivyoko. Vifaa ni lazima vifikie kiwango kifuatacho.

- UMRI WA VIFAA: Kuanzia mwanzoni mwa karne ya 20 hadi sasa, ikiwezekana vifaa vingi viwe kuanzia 1950 kurudi nyuma.
- YALIYOMO: Vifaa sharti viweke kumbukumbu ya historia, jamii, utamaduni, na siasa, na kutilia mkazo haki ya jamii, haki za kibinadamu, na jamii ambazo hazijasajiliwa.

- KUANGAZIA NCHI KULINGANA NA JIOGRAFIA: Vifaa vinavyotoka maeneo ya nje ya Amerika ya Kaskazini na Ulaya vinapendelewa. Tunawahimiza watu kutoka Afrika, Visiwa vya Karibi, Amerika ya Kilatini, Mashariki ya Kati, Asia ya Kati, Asia ya Kusini na ya Kusini-Mashariki na Oceania watume maombi.
- MUUNDO: Vifaa vinaweza kuwa katika mifumo mbalimbali, ikiwemo vifaa vilivyochapishwa, picha, filamu, sauti zilizonaswa, vitu visivyodumu, na vya kidijitali (ikiwa ni zaidi ya blogu, video za simu ya rununu, kurasa za tovuti, picha za 3D, tepu za sumaku na maudhui ya mitandao ya kijamii).